MUHTASARI WA MAMBO YA KUFANYA NA SERIKALI NA VIONGOZI WA KIJIJI

Mabadiliko ya Kisera	**Sera ya Ardhi**: Kutunga sheria ndogo ya kijiji inayotaka kuwa ni lazima kutenga maeneo maalumu ya ardhi kwa ajili ya kilimo, viwanda na biashara. **Sera ya Vijana**: Iwe ni lazima kuwa na Jukwaa la Vijana wote bila ubaguzi.
Mabadiliko ya Sheria na Kanuni	**Sheria ya Ardhi**: Mkutano Mkuu wa Kijiji kuidhinisha sheria ndogo inayotaka kutenga maeneo maalumu ya ardhi kwa ajili ya shughuli za Uchumi kwa Vijana. **Mfuko wa Maendeleo wa Vijana**: Mkutano Mkuu wa Kijiji kupitisha sheria ndogo inayotaka sehemu ya mapato yake kutengwa kwa ajili ya miradi au Elimu ya Ujasiriamali kwa Vijana. **Maeneo ya Masoko**: Serikali ya Kijiji kusimamia sheria ya Masoko inayotaka shughuli zote za kuuza na kununua mazao zifanyike katika maaneo maalumu na kutumia vipimo maalum vya ujazo na uzito. Vijiji vitazuia matumizi ya “Rumbesa”.
Mshikimano wa Taasisi Kuwasaidia Vijana	**Vikundi vya Kuweka na Kukopa**: Serikali ya Kijiji itahamasisha kuundwa kwa makundi ya kiuchumi ya Vijana, Kujenga tabia ya kuweka akiba na kukopa kupitia VICOBA na SACCOS na kuwaunganisha na Taasisi za Kifedha. Kijiji kitakuwa tayari kutumia raslimali zako kudhamini mikopo ya Vikundi vya Vijana. **Kuhamasisha Asasi mbalimbali kutoa Elimu ya** Ujasiriamali kwa makundi ya vijana ili kuwapa stadi za kufanikisha miradi ya kiuchumi. **Kuwaelemisha Vijana juu ya faida ya mifumo mbalimbali** kama vile stakabadhi ghalani ili kuongoza faida ya mazao wanayolima. **Kusaidia Jukwa la Vijana Kijijini kuunganisha nguvu** na Majukwaa mengine ngazi za juu. Kuwafundisha vijana kutumia simu kupata Taarifa za Masoko na Maarifa ya Teknolojia
Vijana Kuwa na Mtazamo Chanya wa Kilimo-Biashara	**Kuanzisha Vikundi vya Sanaa na Utamaduni na Kuwa na Kituo cha Jumuia** ili vijana kupata Elimu ya Kilimo Biashara kupitia sanaa za maonyesho, magazeti, vitabu, redio na runinga. **Kuwaelimisha Wazazi** juu ya wajibu wao wa Kuwasaidia Vijana Kuanzisha miradi yao **Kuwakaribisha watu waliofanikiwa kwenye kilimo**-biashara kuja kuongea na vjijana kijijini. Kuwapa vijana Elimu ya mazingara na kujikinga na magonjwa hatarishi kama ukimwi.

Serikali ya Kijiji kuzifualia Halmashauri ya Wilaya/ Mji pamoja na Ofisi ya Mbunge ili kuwe na madiliko ya: (a) Sera na Sheria inayotaka Mabenki ya Kibiashara kutenga sehemu ya mapato yao kwa ajili ya sekta ya kilimo au Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (b) kuajiri watumishi wa kutosha kutoa Elimu ya Kilimo-biashara kwa Vijana; (c) Elimu ya Kilimo na Kilimo Biashara kufundishwa shule za msingi na sekondari; (d) Kufungua matawi ya VETA and SIDO katika kila Kata kwa kutumia watu binafsi wenye leseni ya Wakala wa VETA na SIDO; na (e) makampuni binafsi kutenga pesa kwa ajili ya mahusiano mazuri na jamii inayowazunguka kwa kuwalenga vijana.

East Africa Youth Inclusion Program

In partnership with

HEIFER INTERNATIONAL

RESTLESS DEVELOPMENT THE YOUTH-LED DEVELOPMENT AGENCY

Mico EMPOWERING COMMUNITIES

YOUTH ALIVE IT'S TIME TO ACT

The Economic and Social Research Foundation (ESRF)
51 Uporoto Street, Ursino Estate. P.O Box 31226, Dar es Salaam, Tanzania
Mobile: +255-754 780133, +255-655 780233
Tel: +255-22 2926084 - 90
Fax: +255-22 2926083
E-mail: esrf@esrf.or.tz or info@esrf.or.tz
Website: http://www.esrf.or.tz

No. 14/2017 - Swahili Version

ESRF POLICY BRIEF

ECONOMIC AND SOCIAL RESEARCH FOUNDATION www.esrf.or.tz

Uboreshaji wa Mazingira Wezeshi ili Kuongeza Ushiriki wa Vijana Kwenye Sekta ya Kilimo-Biashara Tanzania.

WAJIBU NA MCHANGO WA SERIKALI YA KIJIJI

Imeandikwa na: H.Bohela Lunogelo, Fortunata Makene, Patrick Tuni Kihenzile and Richard Ngilangwa

Utangulizi: Kwa kutambua umuhimu wa vijana kuwa ni nguvukazi muhimu katika Ujenzi wa Taifa, na kuelewa kuwa wengi wao wana shauku ya kushiriki katika shughuli za kilimo na biashara zake, na kwa kutambua kuwa vijana kati ya umri wa miaka 15 hadi 24 wanahitaji msaada maalumu; Hivyo basi:

Serikali ya Kijiji Itapaswa Kusimamia Maswala ya Kisheria na Kisera kama ifuatavyo:

A - Serikali ya Kijiji itapaswa kuwajibika katika kutekeleza mambo yafuatayo:

- ✓ Kutenga maeneo maalumu ya ardhi ya kijiji kwa kushirikiana na Kamati ya Maendeleo ya Kata ili kutumiwa na vijana kwa ajili ya kilimo, viwanda vidogovidogo, maghala na masoko au magulio ya mazao.
- ✓ Kutunga sheria ndogo na kanuni zake za kuanzisha Jukwaa la Vijana Kijijini na Kuweka taratibu za kusikiliza hoja za vijana kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji. Kuwasaidia vijana kushiriki kwenye mikutano ngazi za Kata na Wilaya.
- ✓ Kuwaelemisha vijana juu ya fursa za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana wilayani na kuwasaidia kuanzisha Vikundi vya Kiuchumi.
- ✓ Kuwahamasisha na kuwaunga mkono vijana kuanzisha Vikundi vya Utamaduni vitakavyohamasisha vijana kuchangamkia fursa za kiuchumi kwenye sekta ya kilimo na mnyororo mzima wa thamani.
- ✓ Kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wawekezaji wa viwanda ili kutengeneza ajira za vijana.
- ✓ Kutenga maeneo maalum kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya VETA and SIDO ili kupunguza gharama za vijana kujifunza stadi mbalimbali.

B - Viongozi wa Kijiji na Kata (Madiwani) kuendelea kuwashawishi Viongozi wa Wilaya na Taifa kuanzisha mambo yafuatayo:

- ✓ Kutenga bajeti ya kuanzisha vituo va mafunzo ya stadi na ujuzi wa kilimo cha kisasa, usindikaji wa mazao ya kilimo na biashara.
- ✓ Kuanzisha Dirisha Moja la Ushauri wa Vijana juu ya fursa na kuwawezesha kuanzisha kilimo na kushiriki katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo na biashara.
- ✓ Kuunga mkono kupitisha sheria ndogo za kutenga ardhi kwa ajili ya shughuli za kilimo, viwanda na biashara za vijana.
- ✓ Kusimamia bila kupindisha sheria inayotaka Halmashauri kutenga asilimia 4 ya mapato yake kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (MMV).
- ✓ Kuingiza elimu ya kilimo na biashara ya kilimo kwenye mitaala ya shule za msingi, na sekondari.
- ✓ Kuendesha mashindano ya kiwilaya na kitaifa kuwatambua vijana au makundi ya vijana yanayofanya vizuri kwenye shuguli za kilimo, usindikaji na biashara zake.

Muhtasari kwa Viongozi wa Kijiji

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 imetilia mkazo umuhimu wa kuweka mazingiza mazuri ya kuwawezesha vijana kujihusisha na shughuli za kiuchumi, ikiwemo kilimo cha kisasa na kibiashara. Kwa maana hiyo, Serikali ya Kijiji inatakiwa kuwa mstari wa mbele kuwasaidia vijana wake kupata maeneo ya kulima mazao, kufuga mifugo, kufanya biashara za mazao, na kujenga viwanda vidogovidogo. Uwezeshaji wa vijana kujishusisha na shughuli za kilimo na biashara kutasaidia kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira. Kwa sababu vijana wengi wataweza kujiajiri na kuachana na mipango ya kukimbilia mijini. Kwa bahati nzuri kuna miradi ya serikali na wafadhili kama HEIFER International kupitia mradi wa "Kuwajumuisha Vijana wa Afrika Mashariki katika kilimo biashara" *(East Africa Youth Inclusion Program (EAYIP)*). Mradi huu unatambua umuhimu wa kuchochea ushiriki wa vijana kwenye shughuli za kiuchumi zikiwemo kilimo cha kibiashara na mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo. Mradi utaanza na kata/vijiji vichache teule katika halmashauri za Iringa Vijijini, Kilolo, Mufindi, Mafinga mji, Njombe Mji, Njombe Wilaya, Wanging'ombe, Halmashauri ya wilaya ya Mbeya, Rungwe, Busekelo, na Mbozi.

Hali Halisi ya Changamoto za Ajira kwa Vijana

Takwimu za kitaifa zinaonyesha kuwa theluthi moja ya Watanzania wote ni vijana wa umri wa miaka 15 hadi 35. Sensa ya mwaka 2012 ilionyesha kuwa zaidi ya robo tatu (asilimia 76.2 hadi 79.4) ya vijana kati ya miaka 15 hadi 34 wanategemea shughuli za kilimo kujipatia kipato (angalia Grafu Na.1). Mradi wa Heifa wa Kujuimusha Vijana kwenye Uchumi (EAYIP) unalenga kundi kati ya miaka 15 na 24, ambao pia hutegemea kilimo kujikimu.

Grafu 1-Chanzo Kikuu Cha Kipato Kwa Vijana



Sera za Taifa Kuwawezesha Vijana Kiuchumi

Sera ya Maendeleo ya Vijana inatoa mwongozo wa kuwawezesha vijana kwa kuwabadilisha fikra na kuwapatia ujuzi na stadi za kazi, raslimali na mitaji ili waweze kujishughulisha na kufanikiwa kiuchumi, ikiwemo sekta ya kilimo. Sera zingine za kitaifa zinazohimiza vijana kujihusisha na kilimo biashara ni pamoja na rasimu ya 2017 ya Sera ya Taifa ya Ajira (iko kwenye matayarisho) na Mkakati wa Kitaifa wa Kuwahusisha Vijana Kwenye Kilimo 2016-2021.

Sera hizi zinahimiza serikali kuimarisha miundombinu ya kiuchumi na kijamii ili vijana waweze kutumia vizuri elimu, ujuzi na stadi zao kujiajiri na pia kuajiri vijana wenzao. Kwa mantiki hiyo, serikali ya kijiji ina wajibu wa kutafsiri sera hizo na kutafuta mbinu za kuwawezesha vijana wake kiuchumi kwa kuangalia maliasili zilizoko kwenye kijiji na kata husika.

Je Serikali ya Kijiji na KAMAKA wana Wajibu Gani?

Vongozi wa Kijiji na Kamati ya Maendeleo ya Kata

(KAMAKA) watashirikiana na Diwani na Mbunge kuhakikisha kuwa Halmashauri ya Wilaya inatenga bila kukosa asilimia 5 ya mapato ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (MMV) (4%) na Walemavu (1%) Kuna ushahidi kuwa halmashauri zingine hazipeleki michango yote ya asilimia 4 ya mapato ya ndani kwenye MMV. Jambo hili ni la kisheria ya nchi kwa hivyo inapaswa kutekelezwa bila kutoa kisingizio kuwa "kilichokusanywa hakitoshi kwa shughuli zingine za halmashauri".

Pesa zinazopewa Vikundi vya Vijana, ambao wanachama wao huanzia watu watano, huwa kidogo sana kiasi kwamba hazitosha kuleta matokeo chanya ya kiuzalishaji au kibiashara. Kuna umuhimu wa kubadilisha mkakati ili vikundi vipewe mtaji wa kutosha kuwawezesha kufanya mabadiliko ya kweli kiuchumi na kibiashara. Kuna maoni kuwa ni heri kulenga vikundi vichache vitakavyofanikiwa; kuliko kuvipatia pesa vikundi vingi pesa kidogo kidogo ambazo haziwezeshi kufanya mabadiliko ya kiuchumi. Vijana waliohojiwa na mradi huu wa EAYIP walionyesha kujihusisha na ufugaji wa kuku wa mayai na nyama, mbuzi, nguruwe na biashara za kuuza mazao (pamoja na maziwa) na bidhaa zingine za viwandani kwa ajili ya wanavijiji.

Je Vijana Wanakabiliana na Changamoto Gani?

Katika matayarisho ya huu Mradi wa Kuwajumuisha Vijana (Heifa EAYIP) mwaka 2017, wataalamu wa Shirika la ESRF waliambiwa na vijana juu ya changamoto na matarajio yao katika kujihusisha kwenye kilimo biashara:

(a) Kukosa mitaji ya kupanua kilimo-biashara na kutumia mbinu za kisasa zaidi; (b) Wengine hawakujua kuwa kuna Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (MMV) wa Wilaya au masharti yake. Waliowahi kukopa walisema pesa zinazotolewa ilikuwa kidogo mno kukidhi mahitaji; (c) Elimu na uelewa mdogo wa mbinu na teknolojia ya kilimo cha kisasa na kibiashara, kutambua masoko na kutayarisha miradi inayokubalika na taasisi za kifedha; (d) Kukosa ardhi ya kufanyia shughuli za kilimo-biashara kutokana na sababu mbali mbali ikiwa ni pamoja na mila na desturi; (e) Masharti magumu ya kupata mikopo (kama vile riba kubwa na kuweka dhamana ya mali isiyohamishika); (f) gharama kubwa ya pembejeo na zana za kilimo; (g) vijana kubaguliwa kwenye mgao wa ruzuku ya pembejeo za kilimo; (h) bei ndogo ya kuuzia mazao ambayo haileti faida kwa mzalishaji; (i) kubadilika bei ndani ya msimu ikiwa ndogo mno mara tu baada ya kuvuna; na (j) kuwazuia wakulima na wafanya biashara kuuza mazao nje ya nchi kwa faida zaidi kuliko soko la ndani ya nchi.

Serikali ya Kijiji inatakiwa pia kusaidia kutatua changamoto zingine kama vile: (a) wazazi kukataa kuwasaidia vijana kuanzisha biashara; (b) fikra za vijana wengi kudhani kilimo hakina faida; (c) kukukosa jukwaa au utaratibu wa vijana kutoa na kubadilishana mawazo ya kimaendelo na viongozi wa kijiji na kata. Hii ni pamoja na kuwapa fursa vijana kutoa maoni yao kwenye Mkutano mkuu wa Kijiji.

Matumaini Makubwa ya Vijana Mbele Yetu

Vijana wanapaswa kuchukua fursa ya ongezeko la kasi la watu ambao wanategemea ajira maofisini na viwandani na hawalimi. Hawa wote wanahitaji chakula, matunda, vinywaji, nguo, viatu, nyumba na mawasiliano. Kundi la wafanyakazi wa kipato cha kati na cha juu linazidi kuongezeka, hivyo ni soko zuri kwa bidhaa ambazo vijana wanazalisha au kuuza. Mradi wa umeme vijijini unatoa fursa kuanzishwa viwanda vidogodogo vijijini. Taasisi za kifedha pia zimeanza kuwasaidia wajasiriamali.

Je Serikali ya Kijiji Itawasaidiaje Vijana Wake?

Serikali ya Kijiji inalo jukumu la kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya miradi ya vijana kwenye kilimo, viwanda na biashara. Kuwepo maeneo ya shughuli za kiuchumi kwa vijana ni sharti nyeti na muhimu kama kijiji kweli kinakusidia kuwasaidia vijana wake wajiingize na kufanikiwa katika kilimo-biashara. Viongozi wa Kijiji wawasaidie vijana kuanzisha makundi ya kiuchumi na kuunda Jukwa la Vijana ili kubadilishana mawazo na viongozi wa Kijiji na Kata. Kijiji kisaidie kuandaa mafunzo ya kuwajengea uwezo vijana kuwa na ujuzi na stadi za kushiriki kwenye kilimo biashara. Vijana wanahitaji kusaidiwa kubadili fikra na kuwa mtizamo chanya kuhusu kilimo biashara. Jambo linaweza kufanywa kwa kutumia Vikundi vya Sanaa za Maonyesho na Ziara za Mafunzo sehemu nyingine nchini na nje ya nchi.